



Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo

1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21-31 OKTOBA, 2024 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 01-10 NOVEMBA, 2024

1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 21-31 OKTOBA, 2024

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kudhoofika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika. Hali hii ilidumisha mwenendo wa ukandamvua (ITCZ) kuelekea kusini na kuwepo katika maeneo ya Ziwa Victoria na sehemu ya magharibi ya nchi. Halikadhalika, Joto la bahari katika eneo la magharibi wa Bahari ya Hindi (pwani ya Africa Mashariki) liliendelea kuwa la juu ukilinganisha na eneo la kusini magharibi mwa Bahari ya Hindi (Kusini mwa Madagascar) na hivyo kuendelea kuimarisha uvumaji wa upepo wa bahari wenye unyevunyevu kutoka kusini mashariki kuelekea eneo la pwani ya nchi yetu na maeneo jirani.

1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21-31 OKTOBA, 2024

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea kuwepo kwa mvua na ngurumo za radi katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, magharibi mwa nchi na nyanda za juu kusini magharibi. Pia vipindi vya mvua vimeripotiwa katika maeneo ya ukanda wa pwani na maeneo machache ya nyanda za juu kaskazini mashariki.

2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 01-10 NOVEMBA, 2024

2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 01-10 NOVEMBA, 2024

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kudhoofika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kuimarika. Hali hii inatarajiwa kudumisha mwenendo wa sehemu ya ukandamvua (ITCZ) kuelekea kusini na kuwepo katika maeneo ya Ziwa Victoria, magharibi ya nchi na nyanda za juu kusini magharibi. Kwa upande mwingine joto la bahari katika eneo la kati ya

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

kaskazini mwa Madagascar na pwani ya Afrika Mashariki linatarajiwa kuwa la juu ya wastani. Hali hii inatarajiwa kupelekea uwepo wa migandamizo midogo ya hewa na hivyo kuimarisha ukandamvua (ITCZ) katika maeneo ya ukanda wa pwani ya nchi yetu.

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 01-10 NOVEMBA, 2024

Kanda ya ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara):

Mvua na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro): Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Mvua zinatarajiwa katika maeneo machache.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Mvua na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa): Mvua na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Mvua zinatarajiwa katika maeneo machache.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro): Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

Imetolewa na;

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz